

SHULE YA SEKONDARI AHMES

KISWAHILI KIDATO CHA KWANZA

KISWAHILI

KAZI YA LIKIZO

1. (a) Elezea sababu tano za kuibuka kwa rejesta katika jamii.
(b) Kwa kutumia mifano taja aina tano za rejesta.
(c) Fafanua dhima saba za rejesta na matatizo matano ya kutumia rejesta.
(d) Fafanua mambo matatu yanayosababisha kuibuka kwa misimu.
2. Watu wengi hupenda kutumia misimu. Bainisha sababu tano za watu kutumia misimu.
(a) Taja aina tatu za misimu na mifano ya misimu unayoifahamu.
(b) Bainisha njia tano zinzotumika kuunda misimu na kutoa mifano kwa kila njia.
(c) Elezea sifa nane za misimu.
(d) Fafanua faida saba za kutumia misimu.
(e) Toa hasara sita za kutumia misimu katika mawasiliano.
3. (a) Taja aina kuu mbili za utata.
(b) Bainisha sababu saba za utata katika lugha.
(c) Eleza njia saba za kuondoa utata katika lugha.
4. Bainisha faida tano za kuhifadhi fasihi simulizi
5. Taja vipera vya fasihi simulizi vinavyowakilishwa na fasili zifuatazo:
 - i. Hadithi zinazoeleza asili ya watu, kitu, tabia, matukio au maumbile_____
 - ii. Majina ambayo watu hupewa au kujipa kulingana na sifa zao_____
 - iii. Semi zinazochoecha jibu la papo kwa papo_____
 - iv. Mashairi ya kimajibizano_____
 - v. Maneno ya mzaha yanayoambatana na vitendo_____
 - vi. Hadithi zinazoelimisha kwa njia ya kejeli na ucheshi_____
 - vii. Ushairi wenye mizani kati ya 6 na 12_____
 - viii. Hadithi zenye wahusika walaghai/maayari_____
 - ix. Semi zinazoeleza ukweli Fulani_____
 - x. Semi zenye maana iliyofichika_____
6. Andika barua kwa mhariri wa gazeti la Mawingu kukemea ajira za watoto. Jina lako ni
Kimata Takima S. L. P 432 Bunda.